BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA WA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kwanza – Tarehe 21 Septemba, 2016.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 30 June, 2016.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Mambo mengine Yanayohusika na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Mambo mengine Yanayohusika na Hayo.

III. MASWALI:

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

3. MHESHIMIWA MIHAYO JUMA N'HUNGA (Jimbo la Mwera) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali imekuwa ikitoa mkazo kwa watu kufanya kazi kwa kujipatia kipato, lakini wafanyabiashara wadogo wadogo wamekuwa wakinyanyasika na kudhalilika hasa wanapo kuwa katika maeneo yao ya biashara, mfano Mwanakwerekwe na Darajani.

Je, ni lini Serikali itaweza kuwawekea utaratibu mzuri ili wasihangaike na huku Halmashauri zetu zinakuwa zikiwatoza kodi.

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

156. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Serikali hutangaza nafasi za kazi na kusema waombaji wawasilishe vyeti vyao na masharti mengine. Lakini kwa kuwa tuna vijana wengi wanaomba kazi na wengine elimu yao ni ndogo na elimu hiyo ndogo kwa kazi iliyotangazwa hata elimu ya darasa la saba au la kumi inafaa lakini matangazo yanatangazwa kwa vijana anayetaka kuomba kwa elimu yoyote ile.

a) Je, Serikali haioni kuwa inawanyima ajira wale wenye elimu ndogo na wao wanaiweza kazi hiyo.

b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa Taaluma kwa waombaji wa ile kazi inayoombewa ili wale wenye elimu ndogo nao wafaidike na Serikali yao.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

10. MHESHIMIWA NADIR ABDUL-LATIF YUSSUF (Jimbo la Chaani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa skuli zote zipo katika mazingira bora yatakayomuezesha kila mwananchi kupata elimu bila usumbufu wowote. Hata hivyo, kukosekana kwa madawati na ubovu wa skuli ya Chaani kunasababisha wanafunzi walio wengi kusoma katika mazingira magumu na yasiostahiki na hivyo kupelekea ufaulu mdogo wa wanafunzi.

a) Ni lini ukarabati wa skuli hiyo utaanza kufanyika.

b) Serikali imejipanga vipi katika kuwapatia madawati wanafunzi ili kuondokana na changamoto inayoendelea hadi hivi sasa katika skuli hiyo.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

43. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetimiza ahadi yake ya kulipa pencheni kwa wazee waliofika umri wa miaka 70.

a) Je, ni wazee wangapi waliolipwa pencheni hiyo kati ya wazee 21,000 waliopaswa kulipwa.

b) Je, ni wazee wangapi waliokufa kabla ya malipo kuanza na hatu gani zimechukuliwa.

c) Je, Serikali imejipanga vipi kuongeza kima cha pencheni cha 20,000/= ikizingaitiwa kwamba wazee hawa wanamahitaji mengi.

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko:

77. MHESHIMIWA SHADYA MOH'D SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Tumeona hivi karibuni Maafisa Biashara wakitembelea madukani kukagua vyakula ambavyo vimemaliza muda kwa matumizi ya binaadamu, jambo ambalo Serikali inastahili pongezi.

Je, Mhe. Waziri anafahamu kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara hao wasiokuwa waaminifu hubadilisha pakeji na kuweka pakeji nyengine ili kudanganya tarehe sahihi ya kumaliza muda wa matumizi ya bidhaa.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

41. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Vyama vya Michezo vilivyosajiliwa chini ya Wizara yako kwa mujibu wa sheria huwa vina jukumu la Kisheria kufanya marejesho kila baada ya miezi mitatu.

a) Je, ni mara ngapi ZFA wameshawasilisha Wizarani kwako ripoti ya kila miezi mitatu tokea waliposajiliwa.

b) Je, ni vyama gani vyengine vya Michezo vilivyosajiliwa ambavyo havirejeshi marejesho.

c) Je, ni vyama vingapi vilivyo sajiliwa vinavyorejesha marejesho kwa wakati.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

68. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikichukuwa jitihada za kupambana na wadudu wanaoshambulia mimea na matunda kama vile embe, kunde, tungule na inapelekea wananchi wengi kutofanikiwa katika uvunaji wa mazao hayo kwa kutokuwa na uwezo wa kununulia dawa za kuulia wadudu hao.

Je, Serikali inawasaidia vipi wananchi hao katika kukabiliana na tatizo hili.

166. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa hivi sasa watu wengi wameonesha dhamira ya kulima kwa kasi kilimo cha viungo kama kungumanga, hiliki na vyenginevyo.

Je, Serikali ina mpango gani katika kuwatafutia masoko ya nje na ndani wakulima ili kunufaika na kilimo hicho.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

192. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Wananchi wa kijiji cha Paje wamelipa gharama za kuunganishwa umeme tangu mwaka 2015 lakini mpaka leo hii wameshindwa kupata huduma hiyo wakati umeme ni nguzo ya uchumi kwa wananchi masikini katika kuongeza kipato cha kujiajiri.

a) Je, ni sababu gani mpaka leo hii washindwe kuunganishiwa umeme pamoja na kulipa gharama za kuunganishiwa umeme.

b) Je, ni muda gani mtu anatakiwa kupelekewa huduma hiyo ya umeme tangu alipolipa na mnawaeleza nini wananchi hao ambao wanasubiri umeme usiofika.

c) Je, kwa kuwa wananchi hao walitarajia kuvuta umeme na kutumia katika shughuli zao za kiuchumi, mtawalipa fidia kiasi gani baada ya shughuli zao kukwama.

Wizara ya Afya:

56. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Naipongeza sana Serikali kwa jitihada zake kuhakikisha kuwa Jimbo la Mgogoni lililopo Wilaya ya Wete linaimarika katika huduma zake za afya kwa kujenga vituo vitatu vidogo vya afya na kituo kimoja kikubwa ambacho pia hutoa huduma ya mama na mtoto na kujifungulia akina mama wajawazito katika Shehia ya Finya.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kujenga nyumba ya daktari ili kupunguza usumbufu kwa madaktari na wagonjwa na lini nyumba hiyo itajengwa.

132. MHESHIMIWA ALI KHAMIS BAKARI (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Afya ni sehemu ya maisha ya binadamu ambayo sasa kuna ongezeko kubwa la matumizi ya Kondomu jambo ambalo linaongeza hali ya kuchochea ngono na kuwafanya vijana waharibike zaidi.

Je, ni hatua gani za kisheria zinachukuliwa kutokomeza matumizi ya kondomu.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Mambo mengine Yanayohusika na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar, **(Mussa Kombo Bakari)**
21 Septemba, 2016. **KNY. KATIBU WA BARAZA.**